**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA

**Kumb. Na. AB.03/117/01/VOL.II/02** **02 Julai, 2024**

### TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Barua yenye **Kumb. Na. FA.228/613/01/C/041** ya **tarehe 21 Mei, 2024.** Hivyo, anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi zifuatazo:

**1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III – NAFASI MBILI(2)**

**1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA..**

Waombaji wanatakiwa wawe wenye Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Sita (Form Six) aliyehitimu astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.1.1 KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI**

i. Afisa Masuuli na Mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji
ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji
iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
iv. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji;
v. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji;
vi. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
vii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;

S.L.P 44, BUCHOSA-SENGEREMA, Simu +255 (026) 2963630, Nukushi +255 (026) 2963629,
Barua pepe: ded@buchosadc.go.tz, Tovuti: www.buchosadc.go.tz

viii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji;
ix. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka zakijiji;
x. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji;
xi. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
xii. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za kijiji; na
xiii. Atawajibika kwa Mtendaji Mkuu wa Kata.
xiv. Pamoja na kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri wake

**1.1.2 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B.**

**2.0 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;
ii. **Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.**
iii. Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha” Result Slip”,” Statement of Results”,” Provisional Results” au” Transcripts **HAVITAKUBALIKA.**
iv. Kwa Waombaji waliosoma nje ya Nchi, Elimu ya Kidato cha Nne au Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
v. Kwa waombaji waliosoma Vyuo nje ya Nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).
vi. Waombaji watakokidhi sifa zinazotakiwa ndio watakaoitwa katika usaili.
vii. Barua ya maombi iliyosainiwa na Mwombaji inaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili.
viii. Waombaji wenye mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi yao.
ix. Waombaji watakaowasilisha Taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

x. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

xi. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **09 Julai, 2024**

xii. Maombi yote yatumwe kwenye *mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo;* https://portal.ajira.go.tz/ *(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa* 'Recruitment Portal').

xiii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na

Benson P. Mihayo
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**BUCHOSA**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
# OFISI YA RAIS,
# TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA

**Kumb.Na KMC/L.40/8/131** **03 Julai, 2024**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa Kahama imepata idhini ya utekelezaji wa Ajira Mpya katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa barua yenye Kumb. Na. FA. 97/288/01/09 ya Tarehe 25 Juni, 2024 kutoka kwa Katibu Mkuu ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora.

Hivyo, Mkurugenzi wa Manispaa Kahama anawatangazia Watanzania wenye Sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa Kahama, kuomba nafasi za hiyo.

### 1.0 DEREVA DARAJA LA II- NAFASI (03)

#### 1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha Sita (VI) na awe na ufaulu wa daraja la nne na kuendelea, awe mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani, awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari ( Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au NIT au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

#### 1.0.2 KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA

i. Kukagua Gari kabla na baada ya Safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za Kikazi
iii. Kukusanya na kusambaza Nyaraka mbalimbali
iv. Kujaza na kutunza taarifa za safari katika Daftari la Safari
v. Kufanya Usafi wa Gari.

### 1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali Ya **TGS B** kwa mwezi

### 1.0.4 MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si Zaidi ya Miaka **45** na sio pungufu ya Miaka **18.**

ii. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha kuzaliwa.

iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.

iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.

v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa

vi. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE.

vii. Waomabji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni

viii. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza

ix. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 17 Julai, 2024.

x. ***MUHIMU:*** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472,
**KAHAMA – Shinyanga**

xi. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye Mfumo wa Kieletroniki wa Ajira ***(Recruitment Portal)*** kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz/ anuani

hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Secretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa **“Recruitment Portal”**

xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na;

**MKURUGENZI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA**

**KAHAMA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA**

**Kumb. Na. KGR/BDC/S.2/28/V/146** 01 Julai, 2024

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kufuatia kupokea kibali cha ajira chenye **kumb. Na. FA.228/613/01/C/059** cha tarehe **07.06.2024** kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimbenti ya Utumishi wa Utawala Bora** anawatangiza watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kuomba nafasi ya kazi iliyotajwa hapo chini.

## 1.0 DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 1)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)

ii. Awe na leseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Drivingi Course) yanayotolewa na chuo cha VETA au NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

#### 1.1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;

ii. Kupeleka watumishi kwenye safari za kazi;

iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari;

iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;

v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari; na

vi. Kufanya usafi wa gari.

### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGS B

**MASHARTI YA UJUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini serikalini;
ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
iii. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.
iv. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kuzaliwa, Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
**vi.** Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA**
vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CCA. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
x. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.
**xi.** Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **11 Julai, 2024.**
xii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA,**
**S.L.P 491,**
**BUKOBA.**

vii. *Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielectroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz// (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal')*

Limetolwea na:

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA,**

Fatina Hussein Laay

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA**